UNITED NATIONS CONFERENCE ON TRADE AND DEVELOPMENT

UNCTAD

# WANAWAKE WALIO KATIKA BIASHARA ISIYO RASMI YA MPAKANI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:

## MWONGOZO WA SHERIA NA TARATIBU ZA BIASHARA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO



2021

## HAKI NA WAJIBU WAKO[1,2]

### NI ZIPI HAKI ZAKO?

***Haki ya Usalama wa Mtu***

Mfanyabiashara anatakiwa aweze kuvuka mpaka pasipo kuwa katika hatari ya kufanyiwa vibaya, kunyanyaswa au vitendo vya ukatili vinavyohusiana na jinsia. Mashirika mengi ya Kimataifa yanatoa dhamana ya Haki ya usalama wa mtu. Kwa mfano, Itifaki ya Maputo, iliyotiwa saini mwaka wa 2003 na Mataifa mengi ya Kiafrika, imeweka matakwa kadhaa ya kisheria kuhusiana na wanawake, ikionyesha kuwa kila mwanamke anastahili kuheshimiwa, kustahiwa na usalama kwa ajili ya maisha yao.

***Uhuru wa Kutembea***

Kwa wafanyabiashara toka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawahitaji kibali (viza) ili kuingia Kenya lakini wanahitaji hati halali ya kusafiria. Kenya inavitambua vitambulisho vya kitaifa vya nchi wanachama wa Jumuhiya ya Africa Mashariki (EAC) kama hati halali za kusafiria. Tafadhali unaweza kupata uhakika kutoka mamlaka za Uhamiaji.[3]

***Haki ya Uwazi***

Wafanyabiashara wanayo haki ya kupata taarifa muhimu kuhusiana na kanuni, utaratibu wa biashara, vibali vinavyotakiwa, ushuru, ada na kodi. Taarifa kama hizo na hata mabadiliko ya baadae zinatakiwa zipatikane kwa umma au kuoneshwa kwa wazi hapo mpakani.

***Ushughulikiaji wenye Ufanisi wa Miamala***

Shughuli za kibiashara zinatakiwa kuendeshwa na maofisa forodha kwa ufanisi na kwa wakati. Wafanyabiashara wanayo haki ya kudai stakabadhi ya malipo kwa kila malipo yaliyofanyika.

***Haki ya kubeba bidhaa kwa matumizi binafsi***

Watu wanaobeba viwango vidogo vya bidhaa ambavyo sio kwa ajili ya kwenda kuuza bali ni kwa matumizi binafsi wanayo haki ya kutumia mfumo wa ondoleo la ushuru, kuruzukiwa msamaha wa kodi kwa viwango vidogo vya bidhaa, bila kujali zimetokea nchi gani.

# NI NINI WAJIBU WAKO:

## Kuwa na waraka halali

Kabla hujaanza safari yako unapaswa uhakikishe kuwa unao waraka halali ili kukuruhusiwa kuingia katika nchi nyingine. Hii inaweza kuwa hati halali ya kusafiria, kitambulisho chako cha Kitaifa au hati ya kuvuka mpaka.[4]

## Kufahamu wapi pa kuelekea mara unapowasili mpakani

Wafanya biashara wanapaswa wajizoeze kujua taratibu mbalimbali za kuutumia mpaka na kufahamu ni wapi wanapoweza kupata usaidizi wanapokumbana na changamoto.

## Taarifa ya bidhaa

Ni wajibu wa mfanya biashara kutoa tamko la bidhaa kwa mamlaka za forodha chini ya utaratibu husika wa kibiashara. Kumbuka, kuviepuka vituo vya mpakani, kuficha bidhaa, kutoa chini ya kiwango, na kutokutoa mchanganuo wa bidhaa zako inafikirika kama biashara haramu.

## Bidhaa ilizopigwa marufuku

Wafanyabiashara wanapaswa kutambua orodha ya bidhaa zilizopigwa marufuku ambazo hazipaswi kuingizwa, kuuzwa nje au kusafirishwa kwenda nchi nyingine. Bidhaa hizi zinaweza kujumuisha dawa za kulevya, kemikali zenye viini hatari, silaha, wanyama pori na kadhalika. Tafadhali chunguza utaratibu mahususi unaotawala marufuku hizo. Wafanyabiashara wanaokamatwa wakiingiza au kuuza nje bidhaa hizi hushtakiwa chini ya sheria.

## UVIKO-19

Wafanyabiashara wanapaswa kuchukua tahadhari au kuwa na ufahamu wa hatua za kujikinga na UVIKO-19 zinazohusiana na uvukaji wa mpaka.

- Upimaji wa UVIKO-19 katika kituo cha mpakani au kuonesha cheti kinachothibitisha kutokuwa na UVIKO-19. Wasafiri walio njiani kwa zaidi ya masaa 72 watahitajika kupimwa kwa kipimo cha haraka mara wafikapo Tanzania. Kipimo cha haraka kinagharimu $25 kwa kila msafiri.
- Matumizi ya barakoa, kukaa kwa umbali na mtu mwingine na kuosha mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji safi tiririka.
- Kuwekwa karantini kwa lazima kwa watu wenye dalili za UVIKO-19 kwa gharama zako mwenyewe katika eneo lililoahinishwa na serikali.
- Kujaza Fomu ya Ufuatiliwaji wa Afya katika usafiri wowote na kuiwasilisha kwa mamlaka ya Afya ya Mpakani. Kisha wasafiri watapokea Alama Maalum ya Kiafya (a Unique Health Code – UHC), ambayo wataiwasilisha kwa mamlaka za afya mara wafikapo.




## Rushwa

Wafanya biashara hawapaswi kujaribu kutoa rushwa kwa maofisa forodha ili kuepuka malipo ya ushuru au kupata upendeleo.

## Bidhaa zilizozuiliwa

Wafanyabiashara wanapaswa kuijua orodha ya bidhaa zilizozuiliwa au bidhaa zinazodhibitiwa na kupata vibali na leseni za muhimu. Kulingana na nchi husika, bidhaa zilizozuiliwa ambazo vibali vya kuingiza/kuuza nje vinahitajika vinaweza kujumuisha nafaka, mahindi, matunda na mboga za majani, wanyama hai, maziwa mabichi, vileo, mawe ya thamani, bidhaa za petrol na nyinginezo. Tafadhali angalia taratibu mahsusi zinazotawala zuio hizi. Wafanya biashara wanaopatikana wakiingiza au kuuza nje bidhaa hizi bila kibali wanaweza kushtakiwa kisheria.

## Hatua za kusimamia Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS) na vithibitisho vingine

Wafanya biashara wanapaswa kutambua bidhaa zilizo chini ya utaratibu wa Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS), ambazo hati ya uthibitisho inaweza kuhitajika ili kuthibitisha kuendana na kanuni zinazohusiana na usalama wa vyakula, na afya ya wanyama pamoja na binadamu. Wafanya biashara wanapaswa kuwa na uzoefu wa uhitaji mwingine wowote wa vithibitisho.

**! Sehemu hii hapo chini inaelezea Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa wa EAC. Kumbuka: Utaratibu huu unaweza kutumika tu endapo unafanya biashara na nchi nyingine za EAC kama Kenya. Hauwezi kutumika kama unafanya biashara na nchi nyingine nje ya EAC kwa mfano, kama nchi yeyote ya SADC.**

## JINSI YA KUTIMIA MFUMO WA BIASHARA ULIORAHISISHWA WA EAC

Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa ni utaratibu ulioanzishwa katika Jumuhiya ya Afrika Mashariki kuwawezesha wafanyabiashara wadogo kutoka nchi washiriki wa EAC kufanya biashara na nchi nyingine katika eneo la EAC. Mfumo huu uliorahisishwa, hurahisisha taratibu za kibiashara na hupunguza gharama za kufanya biashara mipakani. Unaweza kutumia utaratibu huu kama tu unafanya biashara na nchi nyingine mshirika wa EAC, kama Burundi, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini na Uganda. Wafanyabiashara toka Tanzania wanaofanya biashara na Kenya wanaweza kuutegemea Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa wa EAC.

**Fahamu kuwa Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa haupatikani katika mipaka yote ya EAC.**

**Unaweza kutumia Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa wa EAC kama unakidhi vigezo hivi, ilimradi unafanya biashara ndani ya EAC.**

1. Unauza nje au Unaingiza bidhaa ambazo thamani yake ni chini ya $2,000.
2. Bidhaa zako zinastahili kuwa katika orodha ya pamoja ya bidhaa zilizo chini ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa. Orodha inaweza kupatikana toka kwa maofisa forodha kama haijabandikwa katika ubao wa matangazo mpakani.
3. Bidhaa zako zinakubaliana na kanuni ya chanzo cha bidhaa kama ilivyokubaliwa.

**Kama bidhaa zako haziko kwenye orodha ya pamoja ya bidhaa zinazostahili kuhudumiwa chini ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa:**

- Haziwezi kufaidika kutokana na huduma ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa;
- Kama bidhaa zinastahili kupewa upendeleo (bila kodi au ushuru uliopunguzwa) unahitaji kupata Hati ya Chanzo cha bidhaa kabla hujasafiri kwenda mpakani;

Ushuru unaweza kulipwa kama bidhaa zimezalishwa katika nchi zilizo nje ya Jumhiya ya Afrika Mashariki.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## Kanuni za Chanzo ni Zipi?[5]

Umoja wa Forotha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanzishwa mwaka 2005, uliweka biashara huru (isiyolipiwa ushuru) juu ya bidhaa toka nchi wanachama na Ushuru wa Pamoja wa Nje juu ya bidhaa zilizoingizwa toka nje ya Jumuiya. Bidhaa zinazouzwa huru ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima zikubaliane na Kanuni ya Chanzo cha bidhaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kanuni ya Chanzo cha bidhaa inaruhusu kutofautisha bidhaa zilizozalishwa ndani ya eneo za biashara huria au umoja wa forodha na zile zilizozalishwa mahali pengine. Kama bidhaa imezalishwa yote au kwa sehemu ndani ya eneo hilo hilo la biashara huria au umoja wa forodha, zinaweza zikachuuzwa pasipo ushuru ndani ya eneo la biashara huria au umoja wa forodha.

Kanuni ya Chanzo ya EAC inaweka kuwa:

1. Bidhaa lazima ziwe zimezalishwa au kupatikana katika nchi mwanachama wa EAC
2. Bidhaa lazima ipitie uchakatwaji wa kuridhisha kiwandani ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya mnyororo wa thamani unafanyika katika nchi mwanachama wa EAC

**JE, ULIFAHAMU?**

**HATI MAALUM**

- INATUMIKA KWA WALE WANAOFANYA SHUGHULI ZA MUDA, BIASHARA AU KAZI ZA WELEDI ZENYE MALIPO AU BILA MALIPO.
- ZINADUMU KIHALALI KWA MIEZI 3 NA KUHUISHWA MARA MOJA.

# MFUMO WA BIASHARA ULIORAHISISHWA WA EAC HATUA KWA HATUA

## KABLA HUJASAFIRI KWENDA MPAKANI, HAKIKISHA UNAVYO VITU VIFUATAVYO:




UTHIBITISHO WA HATI HALALI YA KIPIMO CHA VIRUSI VYA CORONA (PCR) CHA MASAA 72 KWA NCHI UNAYOINGIA

KIASI CHA KUTOSHA CHA FEDHA ZA KIGENI


HATI ZA KUSAFIRIA KWA AJILI YA NCHI UNAYOINGIA[6]

Nje ya hati za kusafiria za kitaifa, wananchi wa Afrika Mashariki wanaweza kutumia Hati za Kusafiria za Afrika ya Mashariki, hati ya kusafiria iliyoanzishwa kurahisisha uvukaji wa mpaka ndani ya eneo la Jumuiya ya Afrika Mashariki tu.[7]

KITHIBITISHO CHOCHOTE MUHIMU

Hiki kinajumuisha vibali vya kuuza nje/kuingiza kwa ajili ya bidhaa za aina fulani kama bidhaa za kilimo au wanyama ambazo biashara yake imezuiwa au kudhibitiwa; na hati za uthibitisho za **Sanitary and Phyto- sanitary (SPS) certificates** ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinafikia viwango vya usalama wa vyakula na kanuni za kiafya. Taarifa za Bidhaa zinatakiwa ziwasilishwe katika mamlaka zenye uweledi (Wizara ya Kilimo au Shirika la Viwango) ambazo zitatoa hati ya uthibitisho inayostahili.

## MARA UFIKAPO MPAKANI FUATA HATUA HIZI:



Angalia kuwa bidhaa ziko katika mazao/bidhaa zinazostahili kuwa katika orodha ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa.

Jaza Hati iliyorahisishwa ya Chanzo cha Bidhaa na ipigwe muhuri na ofisa forodha katika nchi bidhaa zinakotokea.

Jaza fomu ya Waraka Uliorahisishwa wa Forodha (fomu ya tamko) ili kutoa taarifa ya bidhaa zako ili ziweze kupigwa muhuri na ofisa forodha katika nchi ambayo bidhaa zinatokea.

Kamilisha utaratibu wa uhamiaji unapoingia katika nchi nyingine.

Wasilisha nyaraka zilizopigwa muhuri katika dawati la forodha katika upande mwingine wa mpaka. Kama bidhaa ziko katika orodha ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa, hutatakiwa kulipa ushuru wowote na unaweza kuendelea na safari yako. Lakini unaweza kutakiwa kulipa kodi na ada nyingine: kwa mfano, Kodi ya Ongezeko wa Thamani (VAT) na kodi ya uzalishaji bado vinahitajika chini ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa. Angalia sehemu inayofuata kwa taarifa zaidi

- Dawati la Taarifa za Biashara linaweza likawepo mpakani mwako ili kukusaidia taratibu za Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa.
- Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pia imeanzisha Dawati la Msaada la Jinsia na Vituo vya Taarifa mipakani mwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwasaidia wanawake wanaofanya biashara mpakani

**!** Chukua tahadhari ya huduma zinazotolewa na mtu wa kati na gharama wanazotoza. Kwa mfano, unapaswa ujue kuwa hakuna ada kwa ajili ya kugongewa muhuri hati yako ya kusafiria na mamlaka husika.

## *Juhudi za Usaidizi za Ukanda wa Afrika Mashariki kwa Ajili ya Kuwaendeleza Wanawake. (EASSI) (The Eastern African Sub-Regional Support Initiative for the Advancement of Women (EASSI))*

EASSI ni shirika linalopigania na kuimarisha uwezo wa wanawake katika mashirika ya vyama vya kiraia. Wanapigania usawa wa kijinsia na haki za kijamii kupitia kuwajengea uwezo, utafiti, kuwasiliana na utetezi kwa wanawake.

Wanafanya kazi na wafanyabiashara wasio rasmi wa biashara ya mpakani katika nchi tisa ili:

- Kuzitambua fursa zinazotolewa katika vyombo mbali mbali vya kibiashara vya EAC kama vile Muunganiko wa Forodha na itifaki za Soko la Pamoja.
- Kuwawezesha wanawake kufaidika katika mchakato wa kuwaunganisha kama ilivyo kwa upande wa wenzao wanaume.
- Kuchangia katika kuweka mazingira wezeshi ya biashara kijinsia.
- Kuanzisha muungano wa wanawake wafanyabiashara ya mpakani katika mipaka mbali mbali ya eneo la EAC ikiwa ni pamoja na Muungano wa Wanawake Wafanyabiashara Mpakani Taveta na Muungano wa wa Wanawake Wafanyabiashara Mpakani Holili.

EASSI pia imeanzisha vituo vya taarifa na msaada katika vituo mbali mbali vya mipakani ambavyo vitaatumika kama mahali pa muunganiko kati ya wafanyabiashara wanawake, maafisa wa mpakani na wadau wengine wanaotafuta kushirikiana na wafanyabiashara wanawake.

## *Ushuru ni nini? Kodi ni nini? Kuna ada nyingine yeyote unayopaswa kulipa?*

**Ushuru au Ushuru wa Forodha** ni kodi zilizowekwa na Serikali juu ya bidhaa zinazoingizwa katika nchi husika. Hizi kodi zinapaswa kulipwa kwa mamlaka ya forodha ya nchi inayoingiza. Kumbuka, kama unafanya biashara chini ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa:

- Haupaswi kulipa ushuru wowote,
- Bado utatoa hati ya uthibitisho ili kuthibitisha chanzo cha bidhaa zako (Hati Iliyorahisishwa ya Chanzo cha Bidhaa). Hati Iliyorahisishwa ya Chanzo cha Bidhaa inaweza kupatikana mpakani na bila gharama.

Ushuru wa forodha haupaswi kukanganywa na kodi nyingine. Kwa mfano, Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa hautoi msamaha kwa mfanyabiashara kulipa kodi nyinginezo kama:

**Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT),** aina ya kodi ya mlaji inayotozwa juu ya bidhaa nyingi wakati thamani inapoongezwa. Kama italipwa, VAT inapaswa kulipwa katika nchi ambapo bidhaa zitauzwa.
Fahamu kuwa katika mazingira mengine VAT huwa inarejeshwa. Kiwango cha kodi ya VAT ni 18%. Ijapokuwa, kiwango hiki cha kodi kinaweza kubadilika kila mwaka. Ulizia katika Mamlaka ya Kodi Tanzania kujua viwango vipya vya VAT.

**Ushuru,** ni kodi inayotozwa juu ya bidhaa kama vileo, tumbaku, petroli, vipodozi, vinywaji baridi n.k. Pale inapohusika, Ushuru unapaswa kulipwa katika nchi ambapo bidhaa zitauzwa. Tembelea Mamlaka ya Kodi Tanzania kupata orodha kamili ya viwango vya ushuru vinavyohusu aina mbali mbali za bidhaa.

**Ada za Usimamizi,** inatozwa kwa ajili ya utaratibu fulani kama kupatiwa Hati ya Uthibitisho ya **Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS)** au kwa ajili ya kuingiza muamala kwenye Mfumo Laini wa Data za Forodha (ASYCUDA). Ada ya ASYCUDA ni Dola za Kimarekani 0.80.

## Orodha kaguzi ya nyaraka unazohitaji ili kufanya biashara pasipo kulipa ushuru chini ya Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa wa EAC



**Hati ya Iliyorahisishwa ya Uthibitisho wa Chanzo cha Bidhaa:** Inatoa ushahidi kuwa bidhaa ulizobeba zimezalishwa kikamilifu au zimepatikana katika nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati zikiwa na thamani ya kufikia hadi $2000. Unaweza kupata hati hii katika ofisi ya kituo cha Mpakani kwa Maofisa Forodha, Taasisi ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) au Mamlaka ya Mapato.

- **Tafadhali chukua angalizo kuwa usifanye udanganyifu juu ya thamani ya bidhaa ili upate stahili ya kupewa hati kwa maana hili litakuwa ni kosa.**



**Fomu ya Idara Forodha Iliyorahisishwa (fomu ya tamko):** Inatumika kutoa tamko la taarifa ya bidhaa zinazoonekana kwenye orodha ya bidhaa zinazostahili kushughulikiwa kwa Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa. Unaweza kuipata hati hii katika kituo cha mpakani.



**Hati za Kusafiria:** Kuwa na nyaraka halali ni muhimu ili kukamilisha taratibu za uhamiaji na kuingia nchi jirani. Hii inaweza kuwa hati ya kusafiria, kitambulisho chako cha taifa, au hati yako ya kuvuka mpaka pale ambapo utaratibu wa hati za mpakani unafanya kazi. Kama unafanya biashara ndani ya mzingo wa kilometa 10 kutoka mpakani hauhitaji hati au waraka wowote.



Nyaraka za ziada ambazo unaweza kutakiwa kuzionyesha hapo mpakani:

**Vibali vya Kuuza nje/Kuingiza:** Hivi vinaweza kuhitajika kwa bidhaa za aina fulani, zikijumuisha kwa mfano mazao ya kilimo au wanyama, ambazo biashara zake zimezuiwa au kudhibitiwa. Taarifa za bidhaa hizi zinapaswa zitolewe kwa mamlaka yenye ustadi mpakani, ambayo itatoa leseni inayofaa ya kuuza nje/kuingiza bidhaa.



**Vyeti vya Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS):** Hivi vinaweza kuhitajika kuhakikisha kuwa bidhaa zinakubaliana na kanuni zinazohusiana na usalama wa chakula, na taratibu za afya za wanayama na binadamu. Taarifa za bidhaa lazima zitolewe kwa mamlaka yenye weledi hapo mpakani (kama Wizara ya Kilimo au Shirika la Viwango), ambayo itatoa hati ya uthibitisho inayofaa inayothibitisha kukubaliana na utaratibu uliyowekwa na SPS.

- Nchi wanachama wa EAC wanaweza kukataza uingizaji wa bidhaa Fulani ili kuwalinda wanyama, mimea, binadamu na usalama wa afya. Ni jambo la muhimu kujua ni bidhaa gani zilizopigwa marufuku kabla ya kusafirisha nje au kuingiza nchini. Kupata orodha kamili ya bidhaa zilizopigwa marufuku, temblea mamlaka za mapato ambako bidhaa zitaingizwa na kuuzwa.

- Bidhaa ambazo hazitakidhi vigezo vya ubora zitataifishwa toka kwa mfanyabiashara.

- Jumuhiya ya EAC imeleta pamoja viwango vya ubora vya bidhaa 366. Zaidi ya hilo, nchi wanachama wa EAC wanatakiwa kuzitambua au kuzikubali alama za ubora kutoka katika nchi wanachama wengine wa EAC. Pale mfanyabiashara anapopeleka nje au kuingiza bidhaa zenye alama ya ubora toka Shirika la Viwango la nchi yake, atakuwa huru kufanya hivyo pasipo bidhaa hizo kupitia tena upimwaji wa viwango vya ubora.

## JINSI YA KUTUMIA ITIFAKI YA BIASHARA YA SADC

Ikiwa unafanya biashara na Kenya, hautaweza kutumia Itifaki za Biashara za SADC kwa sababu Kenya sio nchi mwanachama wa SADC. Badala yake Kenya ni sehemu ya Jumuhiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kama unafanya biashara na nchi yoyote ndani ya SADC, unaweza kutumia Itifaki za Biashara za SADC.

**SADC kwa sasa iko katika hatua ya majadiliano ili kuanzisha Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa kwa ajili ya Jumuhiya hiyo.**

Biashara kati ya nchi za SADC iko chini ya utaratibu wa Itifaki ya Biashara ya SADC, ambayo inakusudia kurahisisha na kuleta ulinganifu katika taratibu za forodha kati ya nchi wanachama na kuendeleza ukuaji wa biashara ndani ya eneo. Chini ya Itifaki, Eneo la Biashara Huria la SADC lilianzishwa 2008 na linatoa muingiliano huru wa soko bila ushuru au ushuru uliopunguzwa kwa bidhaa zinazotoka katika nchi za SADC.[8,9]

▹ Unaweza kufadika kutokana kufikia soko pasipo ushuru chini ya Itifaki ya Biashara ya SADC kama bidhaa zako zinakidhi moja ya masharti yafuatayo ya chanzo cha bidhaa:[10]

1. Bidhaa zako zilizalishwa katika nchi mwanachama wa SADC. Hii ina maana kuwa bidhaa yote imezalishwa, imechimbwa, imevuliwa, imezaliwa na kukuzwa, au kuzalishwa kwa kutumia mali inavyotoka katika nchi wanachama wa SADC.
2. Sehemu ya vifaa/mali inavyotengeneza bidhaa yako vimeingizwa toka nje ya eneo la SADC, lakini mali/vifaa hivi vimepitia “ufanyiwaji kazi au uchakatwaji wa kuridhisha” katika nchi mwanachama wa SADC.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

- Mfano wa bidhaa zinazoweza kukubaliana na sheria za chanzo cha bidhaa chini kifungu 1., inajumuisha mboga za majani zilizovunwa katika nchi mwanachama, wanyama waliozaliwa na kukuzwa katika nchi mwanachama, mazao ya uvuvi yaliyopatikana katika maji ya nchi mwanachama, au bidhaa nyingine yeyote ambayo haina malighafi au vifaa toka nje ya SADC.
    - Chini ya kifungu 2., "iliyofanyiwa kazi au uchakatwaji wa kuridhisha" inatafsiriwa tofauti kwa bidhaa tofauti. Kwa nguo na vitambaa, hii inaweza kuhitaji "mabadiliko thabiti" ya aina mbili. Mfano wa kwanza utakuwa kama jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiingiza nyuzi toka nchi isiyo mwanachama wa SADC, na ikigeuza hizo nyuzi kuwa kitambaa, na ikitumia kitambaa hicho kutengeneza nguo, hiyo nguo itakuwa na sifa kuwa imetoka ndani ya eneo la SADC.
    - Shughuli ambazo hazihesabiwi kama ufanyiwaji kazi au uchakatwaji wa kuridhisha zinajumuisha ufungashaji au kubadili ufungashaji, uunganishaji pamoja au uachanishaji, na "kutia nakshi au shughuli za ukamilishaji" juu ya vitambaa kama vile kutia rangi na kutarizi.
    - Ni muhimu kujua kuwa bidhaa zilizopatikana katika nchi siyo sawa sawa na bidhaa zenye chanzo katika nchi. Bidhaa ambazo hazitakidhi sheria ya SADC ya chanzo cha bidhaa zinajumuisha bidhaa zilizonunuliwa katika nchi mwanachama wa SADC lakini zilizalishwa mahali pengine.
    - Kwa mfano, nguo za mitumba ambazo zinaingizwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Marekani na kununuliwa na mfanyabiashara ili kuuza katika nchi nyingine ya SADC hatakuwa amekidhi kanuni ya chanzo cha bidhaa ya SADC. Mfanyabiashara atalipa ushuru wa forodha ambao nchi husika inayoingiza huwa inatoza kwa bidhaa kama hizi.
    - SADC imechukua Kanuni mahsusi za chanzo kwa takriban kila bidhaa. Sheria hizi zinapatikana katika kiambatisho I cha Itifaki ya Biashara ya SADC iliyofanyiwa marekebisho.[11]


▷ Kama bidhaa zako ni stahiki kupata upendeleo wa Eneo la Biashara Huria, unahitaji kupata Hati ya Chanzo ya SADC kabla ya kusafiri kwenda mpakani.

- Inayotolewa na Chama (Chemba) cha Wafanyabiashara.
- Inagharimu kiasi cha Shilingi 25,000 za Kitanzania
- Kama unauza bidhaa nje toka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Zambia au Malawi, unaweza kupata hati hizi toka Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania.[12]
- Kama unauza bidhaa nje toka nchi yoyote ya SADC kwenda Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, unaweza kuzipata hati hizi toka ofisi za mamlaka husika za forodha.

▷ Kama bidhaa zako hazistahili kupata upendeleo chini ya Eneo la Biashara Huru, ushuru wa forodha unaweza kutozwa.

## ITIFAKI YA BIASHARA YA SADC HATUA KWA HATUA

### KABLA HUJASAFIRI KWENDA MPAKANI, HAKIKISHA UNA VITU VIFUATAVYO:




Nyaraka za kusafiria au visa kwa ajili ya nchi unayoingia. Wafanyabiashara toka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawahitaji kuwa na VIZA ili kuingia eneo la SADC lakini wanahitaji kuwa na hati halali ya kusafiria.

Kuwa na uthibitisho wa kipimo cha PCR (kipimo cha ugonjwa wa UVIKO-19) cha masaa 72 kwa nchi unayoingia.


Fedha za kigeni za kutosha

Uthibitisho wowote muhimu kwa ajili ya bidhaa fulani kama bidhaa za kilimo au wanyama ambazo biashara yake imezuiwa au kudhibitiwa; na **Vyeti vya Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS)** ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinakidhi viwango vya usalama wa chakula na kanuni za afya. Taarifa za bidhaa zinatakiwa zitolewe kwa mamlaka zenye weledi (Wizara ya Kilimo au Shirika la Viwango) ambazo zitatoa hati inayostahili.

Hati ya Uthibitisho wa Chanzo cha Bidhaa cha SADC, ili kuthibitisha chanzo cha bidhaa zako.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## MARA UNAPOWASILI MPAKANI FUATA HATUA HIZI:



1. Uwe na Hati ya Chanzo ya SADC iliyopigwa muhuri na ofisa forodha katika nchi bidhaa zinakotokea.
2. Jaza Nyaraka za Forodha (Fomu ya Tamko) ili kukiri uthibitisho wa bidhaa zako na ipigwe muhuri na ofisa forodha katika nchi ambayo bidhaa zinatokea.
3. Kamilisha taratibu za uhamiaji wakati unapoingia nchi nyingine.
4. Wasilisha nyaraka zilizopigwa muhuri katika dawati la forodha katika upande mwingine wa mpaka ulikotokea.
5. Kama bidhaa zako zina sifa ya kuwa na chanzo katika SADC, hautatakiwa kulipa ushuru wowote. Unaweza kutakiwa kulipa kodi au ada nyinginezo. Tazama hapa chini kwa taarifa zaidi.

## *Ushuru ni nini? Je, Kodi ni nini? Je, kuna ada nyingine zozote ambazo unapaswa kulipa?*

**Ushuru au ushuru wa forodha** ni kodi zilizowekwa na Serikali juu ya bidhaa zinazoingizwa katika nchi husika. Hizi kodi zinapaswa kulipwa kwa mamlaka ya forodha ya nchi inayoingiza bidhaa husika.

Kwa biashara baina ya nchi za SADC, bidhaa nyingi zimesamehewa kulipa ushuru wa forodha. Ili kupata upendeleo wa kuolipa ushuru au ushuru pungufu, bidhaa zako lazima zikidhi kigezo cha kanuni ya chanzo cha bidhaa cha SADC ikiambatanishwa na hati iliyopigwa muhuri ya SADC.

Ushuru wa forodha haupaswi kukanganywa na kodi zingine. Kwa mfano, mfumo wa SADC wa Eneo Huru la Biashara (FTA) hautoi msamaha kwa mfanyabiashara kutolipa kodi nyinginezo kama:

- **Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT),** aina ya kodi ya mlaji inayotozwa juu ya bidhaa nyingi wakati thamani inapoongezwa.
- **Ushuru** ni kodi inayotozwa juu ya bidhaa kama vileo, tumbaku, petroli, vipodozi, vinyaji baridi n.k.
- **Ada za Usimamizi** inayotozwa kwa ajili ya utaratibu fulani kama kupatiwa Hati ya Uthibitisho ya **Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS)** au kwa ajili ya kuingiza muamala kwenye Mfumo Laini wa Data za Forodha (ASYCUDA).[13]
- **Kodi nyingine au Ada – kwa mfano, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa inatoza kodi bidhaa ghafi zinazouzwa nje kama Korosho ghafi, ngozi ghafi na ile iliyochakatwa kiasi.[14]**

Mfumo wa Biashara Uliorahishwa (STR) wa SADC.

Mwaka 2017, kwa kibali cha Mawaziri wa Biashara toka SADC, Secretariati ya SADC ilianza kutengeneza Mfumo wa Biashara Uliorahisishwa (STR) kwa ajili ya biashara baina ya nchi wanachama kwa kusudi la kurahisisha ushughulikiaji wa taratibu za forodha, kurekebisha taratibu za forodha ili kuwezesha kushushulikia kwa haraka na kwa urahisi miamala au shughuli za wafanya biashara wadogo. Kuanzia mwezi Juni 2021, Mfumo Uliorahisishwa (STR) wa SADC ulishakamilishwa ingawa bado haujaanza kutekelezwa.[15]

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## Orodha kaguzi ya nyaraka unazohitaji ili kudai msamaha wa kodi au punguzo la ushuru chini ya mfumo wa Eneo la Biashara Huria (FTA) wa SADC




**Hati ya Chanzo ya SADC:** Inatoa ushahidi kuwa bidhaa ulizobeba zinakidhi matakwa ya SADC kwa ajili ya upendeleo wa msamaha wa ushuru.



**Fomu ya Forodha:** Inaonyesha kiwango na thamani ya bidhaa zinazouzwa nje/kuingizwa.



**Nyaraka za Kusafiria: :** Ukiwa na waraka halali ni muhimu kukamilisha taratibu za uhamiaji na uingie katika nchi jirani. Hii inaweza kuwa hati ya kusafiria, kitambulisho chako cha taifa, au hati ya kuvuka mpaka pale ambapo mfumo wa hati ya mpakani umekamilika. Tafadhali tafuta taarifa toka mamlaka za Uhamiaji.

Nyaraka za ziada unazoweza kutakiwa kuonyesha mpakani:



**Vibali vya Kuuza nje/Kuingiza:** Hivi vinaweza kuhitajika kwa bidhaa fulani, zikijumuisha kwa mfano mazao ya kilimo au wanyama na vyakula, ambavyo biashara yake imezuiwa au kudhibitiwa. Taarifa za bidhaa zinatakiwa zitolewe kwenye mamlaka stadi mpakani, ambazo zitatoa leseni zinazofaa za Kuuza nje/kuingiza.



**Vyeti vya Usalama wa Chakula, Wanyama na Mimea (SPS):** Hivi vinaweza kuhitajika kuhakikisha kuwa bidhaa zinatimiza kanuni zinazohusiana na usalama wa chakula, na taratibu za afya ya wanyama na binadamu. Taarifa za bidhaa zinatakiwa zifikishwe kwenye mamlaka stadi ya nchi bidhaa zinakotokea (kama Wizara ya Kilimo, Idara ya Mifugo au Shirika la Viwango) ambazo zitatoa hati inayofaa kuthibitisha kukubaliana na hatua za SPS.

NOTES

[1] Brenton P. et al (2014). Improving behaviour at borders to promote trade formalization: The Charter for Cross-border Traders. Available at: https://bit.ly/2TDkCOC
[2] World bank (2012). basic rights and obligations for traders and border officials. Available at: https://bit.ly/2H0uLne
[3] EAC regulations on the movement of persons. Available at http://meac.go.ke/wp-content/uploads/2018/02/EAC-Book-3.pdf
[4] EAC regulations on the free movement of persons. Available at http://meac.go.ke/wp-content/uploads/2018/02/EAC-Book-3.pdf
[5] The East African Community Customs Union (Rules of origin) (2015). Available at: https://bit.ly/2AFSBPs
[6] Vitammbulisho vya Taifa vinatambulika pia kama hati za kusafiria na Kenya, Rwanda na Uganda na zinaweza kutumika unaposafiri kati ya nchi 3 washirika.
[7] Tovuti ya Jumuhiya ya Afrika Mashariki: https://bit.ly/2FhP2Tt
[8] Southern African Development Community, 2012. Available at https://www.sadc.int/about-sadc/integration-milestones/free-tradearea/ (Accessed 14 May 2021).
[9] Out of the 16 SADC Member States, Angola, the Democratic Republic of Congo (DRC) and Seychelles have yet to join the SADC FTA.
[10] Chilala B and McCllelland M (2009). Guide to the SADC Protocol on Trade, Southern Africa Global Competitiveness Hub. Available at: https://www.satradehub.org/images/stories/downloads/pdf/guides/SADCTradeGuide.pdf
[11] ANNEX I to the SADC Protocol on Trade. Concerning the Rules of Origin for Products to Be Traded Between the Member States of the Southern African Development Community. Available at https://bit.ly/2QGkWKO
[12] Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture website: Available at http://www.tccia.com/tccia/aenean/ (accessed 10 January 2019).
[13] WTO (2013). Trade Policy Review: East African Community. Revision. World Trade Organization. Geneva.
[14] Tanzania Revenue Authority, 2019, Export Procedures, available at https://www.tra.go.tz/index.php/export-procedures (accessed 14 May 2021).
[15] SADC regional Indicative Strategic Development Plan (RISDP) 2020-2030. Available at https://www.sadc.int/files/4716/1434/6113/RISDP_2020-2030_F.pdf

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA